TANGAZO LA SERIKALI NA. 211 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

## SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE YA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 486 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 6

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ndogo ya 6 kwa-

(a) kufuta na kuandika upya kanuni ndogo ya (1) kama ifuatavyo:

"(1) Halmashauri itahakikisha kwamba ada au ushuru unakusanywa wakati wote katika maeneo yake.";

(b) kufuta kanuni ndogo ya (2); na

(c) kubadili mpangilio wa kanuni ndogo za (3) na (4) kuwa kanuni ndogo za (2) na (3) mtawalia.

Marekebisho ya kanuni ya 10

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 10 kwa kufuta maneno "kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni" na badala yake kuweka maneno "wakati wowote".

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza-

(a) katika Sehemu ya Nne kwa kufuta kipengele

cha sita;

(b) katika Sehemu ya Saba, kwa kufuta maudhui ya safu ya tatu ya kipengele cha 6 na badala yake kuweka maudhui yafuatayo:

“ Ndoo isiyozidi ujazo wa lita kumi - shilingi 1,000/=
Kuanzia ndoo ya lita 11 hadi 20 - shilingi 2,000/=”

(c) katika Sehemu ya Nane kwa-

(i) kuongeza maneno “kwa mwaka” mara baada ya tarakimu “21,500/=” zilizopo katika safu ya tatu ya kipengele cha 5; na

(ii) kuongeza maneno “kwa mwaka” mara baada ya tarakimu “100,000/=” zilizopo katika safu ya tatu ya kipengele cha 7; na

(d) katika Sehemu ya Kumi na Tatu, kwa kuongeza maneno “kwa mwaka” mara baada ya tarakimu “50,000/=” zilizopo katika safu ya tatu ya kipengele cha 8(a) na (b).

Dodoma,
10 Januari, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*